**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**

*Simu*: +255-26-2323189

*Barua pepe*: ps@moha.go.tz

*Tovuti*: www.moha.go.tz

Mji wa Serikali - Mtumba,

Mtaa wa Habari/Afya

S. L. P. 2916,

40483 DODOMA.

**9 Disemba 2025**

## TAARIFA KWA UMMA

## KUHUSU MSAMAHA WA MHE. RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, DKT. SAMIA SULUHU HASSAN KWA WAFUNGWA KATIKA KUADHIMISHA MIAKA 64 YA UHURU WA TANZANIA BARA TAREHE 09 DISEMBA, 2025

Tarehe 09 Disemba, 2025 Taifa letu linaadhimisha Miaka 64 ya Uhuru wa Tanzania Bara. Hili ni tukio muhimu na la kihistoria kwa Taifa letu. Katika kuadhimisha sherehe hiyo, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ametumia Mamlaka aliyopewa chini ya Ibara ya 45(1)(a) - (d) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 kutoa msamaha kwa wafungwa kwa masharti yafuatayo:-

1 (i) Wafungwa wote wenye sifa stahiki wapunguziwe moja ya sita ($^{1}/6$) ya adhabu zao wanazozitumikia hivi sasa baada ya punguzo la kawaida la moja ya tatu (1/3) linalotolewa chini ya Kifungu cha 49(1) cha Sheria ya Magereza Sura ya 58. Wafungwa hao sharti wawe wamehukumiwa kifungo cha kuanzia miaka miwili (2) na kuendelea ambao wametumikia robo $^{1}/4$ ya adhabu zao gerezani na wawe wameingia gerezani kabla ya tarehe 15 Oktoba, 2025, isipokuwa wafungwa walioorodheshwa katika sharti la 2(i — xvi);

(ii) Wafungwa wagonjwa wenye magonjwa ya kudumu au sugu ambao wapo kwenye hatua ya mwisho (terminal stage). Ugonjwa

na hatua hiyo uthibitishwe na jopo la waganga chini ya uenyekiti wa Mganga Mkuu wa Mkoa/Mganga Mkuu wa Wilaya isipokuwa wafungwa hao wasiwe wametenda makosa yaliyoorodheshwa katika kipengele cha 2(i – xvi);

(iii) Wafungwa wazee wenye umri wa miaka sabini (70) au zaidi, umri huo uthibitishwe na jopo la waganga chini ya uenyekiti wa Mganga Mkuu wa Mkoa/Mganga Mkuu wa Wilaya isipokuwa wafungwa hawa wasiwe wametenda makosa yaliyoorodheshwa katika kipengele cha 2(i – xvi);

(iv) Wafungwa wa kike walioingia na ujauzito gerezani au wenye watoto wanaonyonya au wasionyonya waliohukumiwa kifungo cha Mwaka mmoja (1) na kuendelea isipokuwa wafungwa hao wasiwe wametenda makosa yaliyoorodheshwa katika kipengele cha 2(i – xvi);

(v) Wafungwa wenye ulemavu wa mwili na akili wasio na uwezo wa kufanya kazi. Ulemavu huo uthibitishwe na jopo la waganga chini ya uenyekiti wa Mganga Mkuu wa Mkoa/Mganga Mkuu wa Wilaya isipokuwa wafungwa hao wasiwe wametenda makosa yaliyoorodheshwa katika kipengele cha 2(i – xvi);

(vi) Wafungwa waliohukumiwa adhabu ya kuwekwa kizuizini (Under President's Pleasure) ambao wamekaa gerezani kuanzia miaka kumi (10) au zaidi.

2. Aidha, msamaha huo usiwahusishe wafungwa wafuatao:-

(i) Wafungwa wanaotumikia vifungo vya nje na wale waliowahi kukiuka masharti chini ya Sheria ya Bodi za Parole Sura ya 400 (R.E 2023) na kurudishwa gerezani kutumikia adhabu zao, Sheria ya Huduma kwa Jamii Sura ya 291 (R.E 2023) na Kanuni za Kifungo cha Nje [The Prisons (Extra Mural Penal Employment) Regulations, 1968];

(ii) Wafungwa waliopatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo gerezani kwa makosa ya uhujumu uchumi, matumizi mabaya ya madaraka, utakatishaji wa fedha, rushwa na usafirishaji au kujihusisha kwa namna yoyote ile na madawa ya kulevya ikiwemo bangi;

(iii) Wafungwa waliopatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo gerezani kwa makosa ya kujamiana, utekaji au wizi wa watoto, kupoka, kuwapa mimba wanafunzi au makosa yoyote yale yanayohusiana na ukatili dhidi ya watoto na kujihusisha kwa namna yoyote ile na biashara haramu ya binadamu;

(iv) Wafungwa waliopatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo gerezani kwa makosa ya unyang'anyi, unyang'anyi wa kutumia nguvu, unyang'anyi wa kutumia silaha, kumiliki silaha, risasi, milipuko au kujaribu kutenda makosa hayo;

(v) Wafungwa waliopatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo gerezani kwa makosa ya kukutwa na viungo vya binadamu;

(vi) Wafungwa wanaotumikia kifungo gerezani kwa makosa ya kujihusisha kwa namna yoyote ile na nyara za Serikali au ujangili;

(vii) Wafungwa wanaotumikia kifungo gerezani kwa makosa ya wizi au ubadhilifu wa fedha za Serikali;

(viii) Wafungwa wanaotumikia vifungo gerezani kwa makosa ya kutoroka au kujaribu kutoroka chini ya ulinzi halali au kusaidia kutendeka kwa makosa hayo;

(ix) Wafungwa wenye makosa ya kujaribu kuua, kujiua au kuua watoto wachanga (Attempt to Murder, Attempt Suicide or Infanticide);

(x) Wafungwa wenye makosa ya ugaidi, uharamia na makosa ya kimtandao
Terrorism, Piracy and Cybercrimes);

(xi) Wafungwa wanaotumikia kifungo cha pili au warudiaji;

(xii) Wafungwa waliowahi kupata msamaha wa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(xiii) Wafungwa waliotenda makosa ya kinidhamu gerezani ambao makosa hayo hayajatimiza miaka mitatu (3) mpaka kufikia tarehe 09 Disemba, 2025;

(xiv) Wafungwa wa madeni (civil prisoners);

(xv) Wafungwa waliopatikana na hatia ya mauaji au kuhukumiwa adhabu ya kifo na;

(xvi) Wafungwa wanaotumikia kifungo cha maisha gerezani.

3. Wafungwa elfu moja na thelathini na sita (1,036) wamenufaika na Msamaha huu ambapo wafungwa ishirini na mbili (22) kati yao wameachiliwa huru leo tarehe 09 Disemba, 2025 na wafungwa elfu moja na kumi na nne (1,014) wamepunguziwa adhabu zao na watabaki gerezani na kuendelea kutumikia sehemu ya vifungo vilivyobaki. Ni matarajio ya Serikali kuwa wafungwa walioachiliwa huru leo tarehe 09 Disemba, 2025 watarejea tena katika jamii kushirikiana na wananchi wenzao katika ujenzi wa Taifa letu na kwamba watajiepusha kutenda makosa ili wasirejee tena gerezani.

**GEORGE B. SIMBACHAWENE**

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**

**9 DISEMBA, 2025**